

5. Baada ya kuingia katika mfumo; bofya kitufe kilichoandikwa "**Huduma Mtandao**" halafu bofya kitufe kilichoandikwa "**Kampuni**"; katika kipengele cha "**Aina ya Huduma**" chagua "**Kuwasilisha mizania ya mwaka na hesabu**" halafu bofya Endelea.

6. Katika sehemu palipoandikwa "**Tarehe ya Ujumuishaji/Mwafaka**" weka namba ya kampuni yako ambayo tayari ilishasajiliwa nje ya mfumo mfano 12345, halafu bofya kitufe cha "**Tafuta(Search)**". Ukishabofya hapo jina la Kampuni na tarehe ya usajili zitaletwa katika mfumo kutoka katika kanzidata ya makampuni. Katika kipengele cha aina ya kampuni chagua aina ya kampuni yako na halafu bofya palipoandikwa, "**Endelea**" kama utapokea ujumbe wa kosa kama vile "**Kampuni yako haijaoneka katika Masijala ya makampuni**", tafadhali wasiliana na BRELA kwa kutumia nambari za simu zilizopo katika ukurasa wa kwanza wa mfumo wa ORS, kwenye kipengele cha "**ORS Msaada wa Kiufundi**"

#### Jaza taarifa za kampuni yako kama ifuatavyo:

Katika kipengele cha Muombaji, jaza "**Kauli ya Uwakilishi**".

Katika kipengele cha "**Taarifa ya Kampuni**".

Jaza "**Tarehe ya Akaunti**"; hii ni tarehe ambayo kampuni yako itakua kila mwaka ikiwakilisha na kulipia "**Mizania ya Mwaka**". Ingiza nambari ya TIN ya kampuni yako uliyokwisha pewa toka TRA, halafu bofya kitufe cha "**CHECK TIN**" ili kuhakiki taarifa yako ya TIN katika kanzidata ya TIN ya TRA.

Katika kipengele cha "**Ofisi ya Kampuni**" jaza taarifa zinazohitajika.

Chini ya "**Shughuli za Biashara**", chagua vipengele "codes" sahihi vya "**ISIC classification**" toleo la nne vinavyohusiana na shughuli ambazo Kampuni yako itafanya.

Chini ya "**Wakurugenzi**", chagua aina ya utu kisheria ikiwa ni "**Mtu wa kawaida (binadamu) – Raia/ Mzawa**" au "**Mwingine**". Kwa Mtu wa kawaida (binadamu) – Raia / Mzawa, chagua "Mwanzo wa Mtu wa Kawaida (ama uraia wake)" iwe "**Mzawa - Mtanzania**" au "**Mgeni**". Wazawa watahitajika kutoa "**Nambari ya Utambulisho Wa Utaifa**" ambapo mtu wa kawaida (binadamu) wa "**kigeni**" atahitaji kuweka "**Nambari ya Pasipoti**" yake. Aidha kwa "**Mtu wa kawaida (binadamu)**" ambaye ni mzawa, utahitajika kuingiza TIN na kuthibitisha kwa TRA kupitia kwenye mfumo wa ORS. sehemu "**Katibu wa Kampuni**", jaza taarifa

sahihi. Chini ya "**Watu ambao wanaweza kuboresha taarifa katika ORS**", jaza taarifa zinazoombwa hapo jaza pia sehemu nyingine kwa maelezo sahihi, kisha bofya "**Endelea**"

7. Katika hatua ya "Weka kiambatisho", bofya kitufe cha "Furahisha" ili uonyeshe "Funga fomu kwa kampuni" chini ya "magazeti", bofya kitufe cha "Pakua" ili kupakua, kuchapisha, na kusaini maeneo husika.

8. Chini ya sehemu ya "Viambatanishi" tafadhali chagua safu sahihi na bofya kitufe cha "Pakua". Tafadhali majina yako na majina ya fomu na miaka ili kuwezesha uandikishaji. Kwa mfano ikiwa inahitajika kupakua Nambari ya Fomu 128 ya mwaka 2010, tafadhali taita jina lake kwa usahihi "Fomu Na 128-2010 - Iliyotengenezwa. pdf"

Baada ya kuwasilisha viambatanisho vyote, bofya "**Nakubaliana na Vigezo na Masharti**", kisha bofya "**Endelea**".

9. Katika hatua ya "**Thibitisha malipo**" bofya kitufe cha "**Endelea**". Maelezo yako yatapelekwa BRELA kwa ajili ya kupitiwa. BRELA itathibitisha kama taarifa uliyoitoa katika fumo wa ORS inafanana na iliyoko kwenye jalada la kampuni yako. Ikiwa kuna makosa utaambiwa kwa njia ya barua pepe pamoja na taratibu za kufanya ili kurekebisha makosa katika jalada la kampuni yako.

#### HUDUMA KWA WATEJA:

0735 331 001, 0735 000003, 0735 331 004

P. O. Box 9393, Dar es Salaam - Tanzania

Tel: +255 22 218 0139, 218 1344,

218 0113, 2180141, Fax: +255 22 218 0371

Email: usajili@brela.go.tz, ceo@brela.go.tz,

Web: www.brela.go.tz



JINSI YA KUPATA CHETI CHA  
USAJILI WA KIWANDA KIDOGO  
AU LESENI YA KIWANDA  
KWA NJIA YA MTANDAO.  
NA NAMNA YA KUINGIZA TAARIFA  
ZA KAMPUNI ZILIZOSAJILIWA  
NJE YA MFUMO WA MTANDAO  
KATIKA MFUMO WA USAJILI  
KWA NJIA YA MTANDAO  
(ORS)

## JINSI YA KUPATA CHETI CHA USAJILI WA KIWANDA KIDOGO AU LESENI YA KIWANDA KWA NJIA YA MTANDAO.

1. Tengeneza akaunti yako ya ORS
2. Bofya kitufe cha **“Huduma mtandao kwa watumiaji waliosajiliwa”** Kama una Akaunti ya ORS
3. Chagua **“Jina la Mtumiaji”** na uingize Jina la mtumiaji.
4. Chagua **“Nywila”** na uingize Nywila yako
5. Bofya kitufe cha **“Sign In” au bofya kitufe cha “Enter” kwenye kibodi.**
6. Bofya kitufe cha **“Huduma Mtandao”**
7. Bofya Kitufe cha **“Leseni ya Kiwanda”** Kumbuka; Nafasi zenye alama ya nyota, zenye rangi nyekundu ni muhimu na lazima zijazwe.
8. Bofya Kitufe cha **“Utoaji wa Cheti cha Usajili/ Leseni ya Kiwanda”** (Issuance of New Certificate of registration/ Licence)
9. Bofya Kitufe cha **“Endelea”**
10. Jaza Kiwango cha Uwekezaji jumla kilichopangwa katika Tzs (**Fedha za Kitanzania**).
11. Bofya Kitufe cha **“Endelea”**
12. Bofya mshale uliyopo kwenye eneo la aina ya Leseni Kuchagua aina ya Leseni unayoomba.
13. Bofya kitufe cha **“Endelea”**
14. Katika eneo la kauli ya uwakilishi oneshwa kama ni Mmiliki, Mkurugenzi, Katibu au Muwakilishi
15. Katika eneo la mmiliki wa Leseni bofya mshale kisha chagua aina ya mmiliki wa Leseni
16. Katika eneo la namba ya Kampuni, ingiza namba ya Kampuni kisha bofya kitufe cha **“tafuta”** (Search)
17. Katika eneo la jina la shughuli bofya mshale kisha chagua aina ya shughuli.
18. Katika eneo la bidhaa, bofya neno nyongeza kupata nafasi ya kuandika bidhaa itayozalishwa au itayotengenezwa.

19. Katika eneo la kiwanda bofya **“location 1”** kupata mshale wa kuchagua Mkoa, Wilaya, namba ya hati miliki na nafasi ya kujaza maelezo ya eneo fano:- Karibu na kituo cha mabasi Gongo la Mboto.
20. Katika eneo la uwezo uliopangwa, bofya **“capacity”** kupata nafasi ya kujaza bidhaa, kuchagua kipimo mfano Kg n.k, kujaza uwezo uliopangwa wa kuzalisha kwa Mwaka na bei ya kiwandani kwa bidhaa inayozalishwa.
21. Katika eneo la Mpango wa Malighafi (**vifaa vilivyopangwa**) bofya mshale kuchagua mahali yanapotoka malighafi. Mfano ndani ya Tanzania, Nje ya Tanzania, Ndani na nje ya Tanzania)
23. Katika eneo la Mpango wa Malighafi (**vifaa vilivyopangwa**) bofya ndani ya Tanzania (Local) kama malighafi zinatoka ndani ya Tanzania, kisha jaza aina ya malighafi, chagua aina ya kipimo, Eneo kunakotoka malighafi, jaza kiasi cha malighafi na jaza bei ya malighafi, kisha bofya kitufe cha hifadhi
24. Katika eneo la Mpango wa ajira (**ajira iliyopangwa**), jaza idadi ya watanzania na wageni walioajiriwa, kisha bofya kitufe cha hifadhi
25. Bofya kitufe cha **“Endelea”**
26. Chagua (pata) **“kukubali vipengele vya makubaliano ya faragha na uwajibikaji.”**
27. Kupata fomu ya **“Consolidated Application Form”**, bofya kitufe cha **“Pakuwa”** kutoka kwenye sehemu ya chapa **“Printouts Part”**, Kisha, Chapisha, Saini, Pakia fomu kama kiambatanisho.
28. Chagua **“Aina ya kiambatanisho”** bofya mshale kisha chagua aina ya nyaraka ya kuambatanisha.
29. Bofya kitufe cha **“Pakia”** na bofya **“chagua jalada”** kutokea kwenye boksi la **“pakia kiamatanisho”**
30. Katika eneo la **“Chagua aina ya kiambatanisho”** **“bofya mshale na chagua aina ya nyaraka yakuambatanisha.**
31. Bofya mara mbili **“nyaraka yakupakia”**
32. Bofya kitufe cha **“Endelea”**.
33. Chagua **“njia ya malipo”**.

34. Bofya kitufe cha **“Malipo”**.
35. Kupata Ankara ya malipo bofya Kitufe cha **“Pakuwa”**
36. Kuwasilisha maombi kwa msajili wa Viwanda bofya kitufe cha **“Endelea”**
37. Bofya kitufe cha **“Maombi”**.
38. Bofya kitufe cha **“Tazama”**.
39. Kupakua leseni Bofya kitufe cha **“Pakuwa”**
40. Bofya kitufe cha **“Chapisha”**

## NAMNA YA KUIINGIZA TAARIFA ZA KAMPUNI ZILIZOSAJILIWA NJE YA MFUMO WA MTANDAO KATIKA MFUMO WA USAJILI KWA NJIA YA MTANDAO (ORS)

Tunapenda kuwataarifu wapendwa wateja wetu na umma kwa ujumla kuwa Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeanza kutumia mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS). Kutokana na mabadiliko haya tunapenda kuwataarifu wamiliki wa makampuni yaliyosajiliwa nje ya Mfumo wa Usajili (ORS) kuwa wana **wajibu** kuhakikisha kuwa taarifa za makampuni yao zimehakikiwa na zimeingizwa katika mfumo huu wa Usajili Kwa Njia ya Mtandao kwa kutumia utaratibu ufuatao.

1. Ingia kwenye Mfumo wa Usajili Kwa Njia ya Mtandao kwa kutumia anuani ya <https://ors.brela.go.tz/ors> ama kwa kupitia tovuti ya Wakala ambayo ni: [www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz)
2. Kama bado hauna akaunti kwenye mfumo huu wa ORS; bofya kitufe chenye maneno **“Tengeneza Akaunti yako ndani ya ORS”** ili uweze kutengeneza akaunti yako katika mfumo huu wa Usajili Kwa Njia ya Mtandao.
3. Baada ya akaunti yako kutengenezwa utapokea ujumbe kwenye barua pepe yako yenye Jina la Mtumiaji la kilitumia katika mfumo huu, anzisha matumizi ya akaunti yako kwa kutumia taarifa zilizopo katika barua pepe hiyo.
4. Ingia katika mfumo wa ORS kwa kubofya kitufe kilichoandikwa **“Huduma Mtandao kwa Watumiaji Waliosajiliwa”** kwa kutumia **“Jina la Mtumiaji”** ulilotumiwa barua pepe ingiza neno la siri (nywila) uliyoiweka au uliyoweka wakati wa ketengeneza akaunti yako katika Mfumo.